# UBUGUMA BWE’MISORE YEKIFULIIRU U.S.A.

Umoja wa vijana wa kifuliiru nchini marekani almaarufu “UBUGUMA BWE’MISORE YEKIFULIIRU U.S.A”, ni umoja usio wa kiserikali wenye makao yake makuu mjini Indianapolis, Indiana nchini Marekani. Nia na madhumuni ya umoja wetu huu ni Pamoja na kujenga jumuiya miongoni mwa jamii la vijana wa kifuliru wanaoishi Marekani; kuhimiza vijana wetu kujiendeleza kielimu, kutatua matatizo madogo madogo yanayo kumba vijana wetu; kuhamasisha vijana kujitolea katika ujenzi wa jamii letu la wafuliiru hapa Marekani; kutoa huduma, usaidizi na maelekezo ya stadi za Maisha ya hapa marekani kwa vijana wapya wa kifuliru wanaowasili Marekani kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na nchi nyinginezo.

Ikumbukwe ya kwamba makao makuu yetu yatakua yanahamishwa kufuatana na kiongozi aliechaguliwa anapoishi.

## SHERIA NA MIONGOZO

Sheria na miongozo ifuatayo ndio itakayo saidia kuongoza umoja wetu wa Vijana wa kifuliiru hapa Marekani Ili pasije kukajitokeza tafsiri mbali mbali katika uendeshaji wa umoja wetu.

Kama tunavyojua sote umojawetu unajulikana kwa jina la “UBUGUMA BWE’IMISORE YE KIFULIIRU U.S.A” hakuna mtu yeyote bila haki miliki atakaye weza kutumia jina hili kwa faida zake binafsi bila idhini ya viongozi husika.

Baadhi ya vipengele vitakavyo jadiliwa katika sheria hizi ni pamoja na:

i. Wanachama
ii. Wanachama wapya
iii. Michango
iv. Faida za kuwa mwanachama
v. Mikutano ya kamati kuu na wanamemba kwa ujumla
vi. Mitandao yetu ya Kijamii
vii. Uchaguzi wa viongozi
viii. Hatua za nidhamu
ix. Miradi na maendeleo ya umoja
x. Hitimisho (conclusion)
xi. Makubaliano (Agreement)

## I. WANACHAMA

Mwanachama wa Ubuguma Bwe’misore ye Kifuliiru U.S.A ni kijana yeyote yule Mwenye asili ya kifuliiru anaeishi nchini hapa Marekani na awe ameorodheshwa katika kitabu cha wanachama wa ubuguma bwe’misore yekifuliru U.S.A; anae toa michango ya uanachama na kushughulika na majukumu ya ndani na nje ya Buguma bwe’misore yekifuliru hapa Marekani.

Wanachama wa ubuguma bwe’misore ye kifuliiru U.S.A wanagawanyika katika makundi yafuatayo:

**a.** **Wanachama kamati:** Wanachama viongozi ni wanachama wanao simamia kamati ya uendeshaji na uongozi wa ubuguma bwe’misore yekifuliiru U.S.A, kwa mfano president, v/c president, na kadhalika.

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

**Wanachama wote kwa ujumla:** Ni wanachama wa kawaida wote kwa ujumla wanao toa michango na kuhusika na shughuli za ndani na nje ya ubuguma bwe'misore yekifuliru U.S.A ila ambao sio viongozi.

## II. WANACHAMA WAPYA

Tunapopata wanachama wapya ambao wanataka kujiunga katika umoja wetu wa Ubuguma bwe'misore yekifuliiru Marekani, vigezo vifuatavyo lazima vizingatiwe.

Kamati ya uongozi itapewa taarifa na mawasiliano ya ndugu anae taka kujiunga na umojawetu, msemaji wetu mkuu atawasiliana na ndugu huyo na kumsikiliza na kumpa taarifa, kanuni na misingi ya umoja wetu. Ndugu huyo ni lazima awe mkaaji wa hapa Marekani, awe Mufuliiru wa baba na mama ao baba, na awe ametimiza umri usiozidi miaka kumi na minane(18) Msemamaji wetu atakapomaliza kuongea nae, atawasilisha taarifa zake kwenye kamati kuu na kamati ikiridhika, ndugu atatumiwa fomu ya usajili na kukaribishwa katika umoja wetu.

Mtu yeyote anaye omba kuwa mwanamemba ao kama tayari ni mwanamemba anaweza akakataliwa uanamemba ao uanamemba wake unaweza kusitishwa iwapo itabainika ao kuzibitishwa yakwamba ndugu huyo:

- Sio mkaaji wa Marekani
- Sio mufuliru wa asili ya baba na mama
- Sio mufuliru wa asili ya baba.

Mwanachama anapo amua ku left kundi bila sababu yeyote kwa mda wa miezi miwili bila kutaarifu uongozi sababu ya kuondoka kwake, iwapo ataamua tena kurudi kwenye kundi atatakiwa kutowa $100 ili aruhusiwe kurudi kwenye umoja wetu.

## III. MICHANGO

Kama desturi na kawaida yetu kila mwanachama kiongozi ao asiyekuwa kiongozi alie orodheshwa katika kitabu chetu cha uanachamana atakua anatoa mchango usiozidi $150 kwa mwaka. Mchango huo utatolewa kwa kupelekwa kwa mlinda hazina wetu ao unaweza kuwa deposited katika account ya ubuguma bwemisore yekifuliiru itakapo imarishwa.

Nilazima kila mwanachama awe anatoa mchango wake wa kila mwaka kwa uendelezi wa ubuguma. Na ikumbukwe ya kwamba mchango huu ndio unao kuimarisha wewe kuwa mwanachama. Mchango huu utakua ukipokelewa kuanzia mwezi wa kwanza hadi wa tisa, ianahitajika kufika mwezi wat isa kila mwanamemba ameisha wakilisha mchango wake wa mwaka. Unapotoa mchango wako fahamu ya kwamba hauwezi ukarudishwa kwa sababu yoyote ile. Tofauti na michango yetu hii ya mwezi vile vile tunayo michango ya dharura ambayo itakua inajitokeza iwapo mmoja kati ya wanamemba wetu anapatwa na dharura zifuatazo;

- Kilio (vilio) kila mwanamemba atachangia $100
- Graduation kila mwanamemba atachangia $25
- Kuowa ao kuolewa kila mwanamemba atachangia $50
- Mchango wa mkutano wa kila mwaka $100

Michango yote ile itakua inatolewa kwa niaba ya ubuguma bwe'misore yekifuliiru U.S.A. na utumiaji mbaya wa michango ya kamati hatua kali itachukuliwa kwa atakae tumia vibaya mali ya ubuguma ikifuatana na kusimamishwa katika shughuli zote za buguma na hata kufukuzwa.

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

# IV. FAIDA KWA WANACHAMA

Faida (misaada) nyingi na tofauti zitakua zikitolewa kwa wanachama wa buguma bwe'misore ye kifuliru U.S.A kufuatana na hali itakayo jitokeza na kufuatana na katiba yetu inavyo sema.

Baadhi ya faida zitakazo tolewa ni pamoja na:

a. Kilio (vilio)
b. Magonjwa
c. Uzazi
d. Kuhitimu shule (graduation)
e. Kuowa na kuolewa
f. Tunapo pata wageni (vijana wapya wa kifuliru wanapo wasili hapa nchini Marekani).

Ili mwanachama anufaike na misaada hii kunavigezo ambavyo vinatakiwa kufuatwa.

**a. Kilio (Vilio)**

Kama tunavyo fahamu sote tuna aina tofauti za vilio; kilio cha mwanamemba kinapo tokea hapa hapa Marekani; kilio kwa mwanamemba toka nyumbani Africa.

i. **<u>Kilio kwa mwanamemba kinapo tokea hapa hapa Marekani</u>**

tutakapo mpoteza mwanakamati (mke, mme, single) hapa kwetu Marekani kila mwanachama atachangia $100. Pesa hizo zitasaidia katika mipango na maandalizi yote ya kilio; Kamati itawasiliana na familia na wasimamizi wa msiba huo na kuwakilisha pesa hizo ili zisaidie katika maandalizi ya msiba huo. Kilio kitakapo kwisha kamati itakutana na kujadili matumizi ya pesa hizo ilivyo kwenda. Mwanamemmba atakapo mpoteza Mtoto wakujizalia, baba ao mama mzazi, kila mwanamemba atatoa $50 zitakazo tumwa kwa mwanamemba na kumsaidia katika kipindi hicho kigumu atakachokua anapitia.

ii. **<u>Kilio kutoka Africa na maeneo mengine.</u>**

kilio kwa mwanamemba ambacho kimetoka Africa na maeneo mengine kitakacho kua kinashughulikiwa ni iwapo mwanachama atakua amepoteza ndugu wafuatao;

baba ao mama mzazi, mtoto wako wakujizalia, mme ao mke wako wa ndoa.

Hao ndio watu kilio chao kitashughulikiwa. Iwapo mwanachama atapoteza mmoja wao.

Kilio hicho kitakapo jitokeza kitashughulikiwa kama ifuatavyo; $25 zitatozwa kwa kila mwanamemba na kupatia mwanachama aliye mpoteza ndugu kwa ajili ya maandalizi ya msiba.

Ili mwanamemba aliyefariki hapa Marekani aidha kufiwa na mtu hapa Marekani aidha kutoka nje ya Marekani anufahike na hayo yote yaliyotajwa hapo juu lazima vigezo vifuatavyo viwe vimetimizwa na mwanamembahuyo aliye fariki ao kufiwa. Vigezo hivyo ni kama vifuatavyo:

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

- Awe ameorozeshwa kwenye kitabu cha wanamemba
- asiwe na deni yoyote kwenye ubuguma.
- awe anahuzuria kwenye vikao, na kushughulika na mambo ya ndani ya buguma.

Mwanakamati atakapo poteza ndugu yeyote ule tofauti na walio tajwa hapo juu umoja wetu hauta toa msaada wowote ule, ila tutaungana sote kwa pamoja na kumfariji.

**b. Magonjwa**

Magonjwa yanapo jitokeza kwa mwanamemba tafadhali julisha viongozi ili wasambaze Habari ya kwamba tunaye mgonjwa katika familia zetu, ili atakae kuwa na mda afike kuangalia hali ya mgonjwa. Iwapo magonjwa yataendelea kwa kipindi kirefu aidha iwapo magonjwa yake yatabainika ya kwamba yamekua sugu na kumzuia kuendelea na shughuli zake za kawaida, kamati itakaa chini na kuangalia jinsi ya kumsaidia. Na iwapo kamati itaamua ya kwamba ndugu asaidiwe msaada huo usizidi $300 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Ili mgonjwa anufaike na msaada huo ni lazima:

- Awe ameorozeshwa kwenye kitabu cha wanamemba
- asiwe na deni yoyote kwenye umoja wetu.
- awe anahuzuria kwenye vikao, na kushughulika na mambo ya ndani ya buguma.
- Awe amekaa katika umoja kwa kipindi kisichozidi miezi sita (6)

**c. Uzazi**

Mwanamemba anapo jifungua $150 zitatolewa katika mfuko wa hazina na kuziwakilisha kwa ndugu alie jifungua kama zawadi kwa kuliongeza jamii letu la wafuliru.

Ili mzazi anufaike na msaada huo ni lazima:

- Awe ameorozeshwa kwenye kitabu cha wanamemba
- asiwe na deni yoyote kwenye umoja wetu.
- awe anahuzuria kwenye vikao, na kushughulika na mambo ya ndani ya buguma.
- Awe amekaa katika umoja kwa kipindi kisichozidi miezi tisa(9)

**d. Kuhitimu Shule**

Mwanamemba anapokaribia kuhitimu shule tafadhali toa taarifa miezi sita (6) kabla ya tarehe ya kuhitimu ili kuwapa viongozi na kundi kwa ujumla mda wa kuandaa zawadi ya kumuwakilishia mhitimu siku ya graduation. Zawadi zitakua zinatolewa kama ifuatavyo:

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

- PHD   $700
- Master’s $500
- Bachelor’s $300
- Associate $200
- High school $150

Ili mhitimu anufaike na msaada huo ni lazima:

- Awe ameorozeshwa kwenye kitabu cha wanamemba
- asiwe na deni yoyote kwenye umoja wetu.
- awe anahuzuria kwenye vikao, na kushughulika na mambo ya ndani ya buguma.
- Awe amekaa katika umoja kwa kipindi kisichozidi miezi tisa (9)

#### e. Kuowa Na Kuolewa

Mwanamemba aidha wanamemba wanapo amua kufunga pingu za Maisha aidha kwa njia ya harusi ao kwa njia ya mila na desturi zetu, Mwanamemba anaefunga pingu za Maisha atatakiwa kutowa taarifa kwa viongozi husika miezi mitatu kabla, ili umoja ufanye maandalizi ya zawadi itakayo wasilishwa siku ya harusi kama itakuwepo ao nyumbani kwao kama hakuna harusi. Ikumbukwe ya kwamba ndoa itakayo tolewa zawadi ni ndoa ilio unganishwa aidha kwa misingi ya serikali, ao kanisa. Vinginevyo umoja wetu hauta husishwa na ndoa zisizo unganishwa na misingi tajwa hapo juu. Zawadi itakayo tolewa ni Printed and framed 20X30 picture Pamoja na $1000.

Ili mwanandoa anufaike na msaada huo ni lazima:

- Awe ameorozeshwa kwenye kitabu cha wanamemba
- asiwe na deni yoyote kwenye umoja wetu.
- awe anahuzuria kwenye vikao, na kushughulika na mambo ya ndani ya buguma.
- Awe amekaa katika umoja kwa kipindi kisichozidi miezi tisa (9)

#### f. Tunapopata Vijana Wapya Kutoka Nyumbani

Tunapo pokea taarifa za uwepo wa vijana wapya wa kifuliru hapa Amarekani, viongozi wetu watapewa taarifa na mawasiliano ya wageni, viongozi watawasiliana nao na kuwapa taarifa za uwepo wa ubuguma bwe’misore yekifuliiru U.S.A.

## V. MIKUTANO YA KAMATI KUU NA WANAMEMBA WOTE

Mikutano yetu itakua inahudhuriwa na wanachama viongozi na wanachama wakawaida, kawaida tutakua na aina mbili za mikutano.

- Mikutano ya Kamati ya uongozi
- Mikutano na wanamemba wote (assemble general)
- Mkutano mkuu wa Mwaka.

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

**Mikutano ya kamati ya uongozi**: Mikutano hii ni mikutano ya kamati yetu kuu ya viongozi wa ubuguma bwe'misore ye kifuliiru usa wanao kutana kila mara mbili kwa mwezi. Katika mikutano hii viongozi wetu hujadili, na kutaasmini maendeleo ya umoja, kufikiria miradi mipya ya uendelezi wa umoja na kutatua matatizo ambayo yanaweza kua yanakumba umoja wetu.

**Mikutano na wanamemba wote** (assemble general)**:** Mikutano hii nimikutano na wanamemba woote kwa ujumla, mikutano hii hupangwa na kamati ya uongozi na kujulisha wanamemba wiki moja kabla. Mikutano hii itakua ikiongozwa na president ao makamu wake ao kiongozi yeyote atakaye teuliwa na president. Ndani ya mkutano mazungumzo yetu yote yataendeshwa kwa njia ya kidemokrasia na kwa utulivu. shabaa ya mkutano itatolewa na president ao kiongozi msimamizi huku nidhamu ikifuatwa.

Hakuna anaye ruhusiwa kuongea bila ruhusa ya msimamizi wa mkutano. unapotaka kuongea omba ruhusa na hakikisha maongezi yako yanaendana na mada inayo jadiliwa. Mda wa kumaliza kikao utaamuliwa na kiongozi msimamizi.

Mikutano yetu yote hii itakua inaendeshwa kwa njia ya whatsapp group yetu ao accounti yetu ya zoom.

**Mkutano Mkuu wa Mwaka:** Mkutano wetu mkuu wa mwaka ni mkutano ambao utakua unakutanisha wanamemba wote kwa ujumla. Mkutano huu ni wa maana sana kwa sababu utatupatia sisi wanamemba fursa ya kukutana kujuana na kusherehekea kwa Pamoja, vile vile itatupa fursa ya zoezi la uchaguzi wa viongozi iwapo muhula wa watawala utakua umekwisha. Mkutano huu utapangiliwa na kamati ya uongozi, watachagua tarehe na mahali(city, state) ambako mkutano wetu utafanyika na kuutangaza ndani ya assemble general miezi sita kabla.

Baada ya tarehe na mahali kutangazwa kila mwanamemba atatakiwa kuchangia $100 kwa ajili ya maandalizi ya mkutano huu.

Ni lazima kila mwanamemba awe anahudhuria kwenye mkutano huu, na kuchangia kwa ajili ya maandalizi, usipo hudhuria ao kuchangia mara mbili mfululizo Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa ajili yako.

## VI. MITANDAO YETU YAKIJAMII

Mitandao yetu ya kijamii ni sehemu kubwa inayo tuwezesha kujiendeleza kutuunganisha na kutangaza umoja wetu, hivyo basi kama vijana tunatakiwa kuitumia kwa umakini na kwa nizamu. Baadhi ya mitandao umoja wetu unatumia kwa sasa ni Pamoja na;

- WhatsApp
- Facebook
- Instagram
- Zoom
- YouTube

©*2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

**WhatsApp:** Accounti yetu ya WhatsAp ni sehemu inayo cheza kazi kubwa katika kuendeleza umoja wetu na kutukutanisha sote kwa Pamoja. Accounti yetu hii itakua ikiendeshwa na msemaji wetu mkuu Pamoja na mwandishi watu hawa wawili ndio wenye mamlaka ya kuongeza ao kupunguza mtu baada ya kupokea agizo toka kwenye kamati kuu. Kila mwanamemba anahaki ya kuongea ao kutuma ujumbe, kutoa maoni ao pendekezo lolote linalo husika na uendeshaji wa umoja wetu.

Mambo yafuatayo nilazima yazingatiwe pindi tunapo tumia mtandao wetu huu:

- Hairuhusiwi kutuma video, picha ao link yeyote isiyoendana na maadili, mada, ao misingi ya umoja wetu. Unapokua na video ao link ambayo unaona inaweza kua na mafaa kwenye kundi, wasiliana na msemaji wetu mfikishie jambo hilo na ataliwakilisha sehemu husika lichunguzwe na maamuzi kuchukuliwa.
- Heshima kwa sote ni Jamabo la msingi, matani yaliyo pitiliza hayaruhusiwi.
- Emoji sizizo endana na maadili yetu na zakutengenezwa haziruhusiwi.
- Maswala ya mapenzi(kutongozana) hairuhusiwi, endapo wanamemba wawili wataamua kua pamoja basi julisheni viongozi kuhusu mahusiano yenu ila accounti ya umoja isiwe sehem yenu ye mawasiliano.

**Facebook, Instagram & Zoom:** Accounti zetu hizi vile vile zinacheza nafasi kubwa katika uendeshaji na utangazaji wa umoja wetu na biashara zetu. Accounti hizi zinaendeshwa na msimamizi wa media na Maendeleo, vile vile hairuhusiwi kupost jambo lolote lisiloendama na maadili ao sheria za umoja wetu. Kila kitakacho postiwa lazima kiwe Napata approval kutoka kwa viongozi husika, Mambo binafsi haya ruhusiwi kupostiwa kwenye mitandao yetu hii, hivyo basi mitandao hii haitatumika katika misingi ya kujinufaisha binafsi bali kwa manufaa ya Ubuguma bwe'misore yekifuliiru U.S.A.

**ONYO:** Utumiaji mbaya na kutofuata sheria za utumiaji wa mitandao yetu hii yakijamii hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa yeyote yule ikiwa Pamoja na kufukuzwa kwenye umoja.

## VII. UCHAGUZI WA VIONGOZI

Uchaguzi wa viongozi utakuwa ukifanyika kila baada ya miaka minne (3).

Uchaguzi utakua unaendeshwa na kamati yetu ya washauri ndani ya mwezi ambao tumepanga kukutana

Ili uwe mgombea utahitajika:

- Uwe mkaaji wa Marekani
- Uwe na umri wa Zaidi ya miaka 20
- Uwe mtoaji mzuri wa michango ya ubuguma
- Uwe umeisha kaa ndani ya umoja Zaidi ya mwaka mmoja
- Usiwe na deni lolote kwenye kundi

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

- Uwe umehudhuria kwenye vikao vyote vitakavyo fanyika ndani ya mwaka huo wa uchaguzi.

Kiongozi atakae bahatika kutuongoza anaweza kutuongoza kwa mihula isiozidi miwili; hakuna kiongozi aliechaguliwa kidemocratia atakae kaa madarakani Zaidi ya mihula miwili (Zaidi ya miaka sita). Iwapo ikitokea muhula wa kiongozi alie madarakani umekwisha na maandalizi ya uchaguzi hayaja kamilika aidha hakujaonekana mgombea Anaye timiza vigezo vya kua kiongozi, kiongozi alie madarakani atasalia madarakani kwa mpito mpaka pale atakapo patikana kiongozi mya.

## VIII. HATUA ZA NIDHAMU

Hatua za kinidhamu zifuatazo zitakua zikitolewa kwa kila mwanamemba.

- Kuitwa ujieleze
- Kupewa onyo
- Kusimamishwa kuhudhuria shughuli za umoja
- Kufukuzwa

**Kuitwa ujieleze**: mwanamemba ataitwa ajitetee atakapokua:

- Anachelewa kuvikao
- Kutohudhuria vikao
- Kutohesimu sheria

**Kupewa onyo**: mwanamemba atapewa onyo iwapo:

- Atachelewa mara tatu mfululizo kuvikao bila sababu maalum
- Asipotoa mchango kwa Zaidi ya miezi mitatu
- Iwapo atatumia jina la umoja wetu kwa kutaka kujinufahisha bila idhini ya viongozi husika.

**Kusimamishwa**; mwanamemba atasimamishwa iwapo:

- Atakua na usimamizi mbaya
- Asipo toa michango kwa kipindi cha miezi 6
- Asipo support maamuzi na miradi iliyo anzishwa na kamati
- Kuleta vurugu wakati wa vikao
- Asipo zingatia sheria na uratibu wa utawala.

Na mambo mengine yasio endana na uratibu wa kamatiyetu.

**Kufukuzwa:** Mwanamemba atafukuzwa iwapo

- Asipo Heshimu ao kutenda mambo kinyume na katiba ya ubuguma bwi'misore yekifuliiru U.S.A

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

- Akiiba mali ya ubuguma.
- Utumiaji mbaya wa mali ya buguma bila idhini ya Utawala.
- Kutoshughulika na mambo ya ndani ya ubuguma kwa kipindi kisichozidi miaka miwili(2)
- Kutokutoa michango kwa Zaidi ya miaka miwili

## IX. MIRADI NA MAENDELEO YA UMOJA

Miradi ni sehemu kubwa ya kuleta maendeleo na ukuzi wa umoja wetu. Miradi yote itakua inaendeshwa kwa jina la ubuguma bwe'misore ye kifuliiru U.S.A. mradi unapo teuliwa utajadiliwa na kamati kuu ya viongozi na kutangazwa kwa wanamemba wote ndani ya assemble general. Miradi yetu yote itakua ikiendeshwa na mfuko wa kamati yetu huku ikisimamiwa na kiongozi wa projet, secretaire na mlinda hazina.

Ni jukumu la kila mwanamemba kusupoti miradi itakayo kua inaanzishwa na umoja wetu, utumiaji mbaya na kuto supporti miraradi ilioanzishwa na umoja wetu hatua kali yakinidhamu itachukuliwa kwa yeyote ule atakae saliti maendeleo ya umoja wetu.

## X. HITIMISHO (Conclusion)

Wanachama wote wa Ubuguma bwe'emisore yekifuliiru U.S.A wanahitajika kufuata, kuzingatia na kuheshimu sheria na miongozo iliomo kwenye katiba hii kwa uendeleshaji mzuri wa umoja wetu. Sheria hizi zitatumika kwa wanachama wote, viongozi na wasio viongozi. Sheria hizi zinaweza kubadilishwa na wakuu wa kamati mda wowote ila ubadilishaji wake utahitaji asilimia sitini (60%) ya kura za urekebishwaji wa katiba toka kwa wanamemba wote wa ubuguma bwe'misore yekifuliiru U.S.A.

*Sheria hizi zitaanza kazii zitakapo somewa wanakamati wote na kuhidhinishwa na kamati ya viongozi wa ubuguma na asilimia sabini ya makubaliano na wanakamati wote kwa ujumla.*

## XI. MAKUBALIANO (Agreement)

Baada ya kusoma sheria hizi, sisi wanamember tumekubaliana na maneno haya, kuyanzingatia na kuyafanyia kazi.

| MAJINA YA WANA MEMBER | SIGNATURE |
| --- | --- |
| Adela Ngandu | |

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

| MAJINA YA WANA MEMBER | SIGNATURE |
| --- | --- |
| Adeline Juma | |
| Adolphine Maombi | |
| Agnes Bagaluha | |
| Alex | |
| Alexis T Mafuta | |
| Aline Apolina | |
| Aline Apoline | |
| Amos Gentil | |
| Beteli Musafiri | |
| Bienvenu Marko | |
| Bonheur Muhuzi | |
| Busare Reke | |
| Chance Bukuru | |
| Chris Mapenzi | |
| Daniel Shambale | |
| Dieu-Fidele Basimise Munano | |
| Dina Kasigwa | |
| Emmanuel Fataki | |
| Fazili Rajabu | |
| Fidele Bakita | |
| François B. Kulolwa | |
| Freddy Rusimbana | |
| Georgette Shimambo | |
| Gloria Queen | |
| Gretta Kubembeleza | |
| Imani Malgha Baraka | |
| Ismail Makonero Bayuku | |
| Jacques Bulimbi | |
| Jeanne Kabemba | |
| Jules Bakita | |
| Julita Rajabu | |
| Lily Mbambane | |
| Mathayo Reke (Matthias) | |
| Merci Matiabu David | |
| Moise Paulo | |
| Mwavita Rajabu | |
| Nabunyere | |
| Roda Kituza Lazaro | |
| Roger Kongwa | |
| Sara Rajabu | |
| Shebyage Mushalizi Sandowa (Mr. Mkubwa The Mc) | |

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*

| MAJINA YA WANA MEMBER | SIGNATURE |
| --- | --- |
| Shukrani Matabishi | |
| Ujumbe Alex | |
| Zaina Shendera | |
| Zena Mami | |

UBUGUMA BWE MISORE YE KIFULIIRU USA
UMFU

*©2024 Ubuguma bwe Misore ye Kifuliiru USA.*
*All Rights Reserved.*